

2020

CensusMaryland

Muhimu Rahisi na Salama

Marekani inahitajika kufanya hesabu ya taifa ya watu wote wanaoishi katika kila jimbo kila baada ya miaka kumi (Katiba ya Marekani, Kipengee cha 1, Kifungu cha 2).

Sensa ya 2020 inaathiri Maryland kwa njia mbalimbali muhimu.
Sensa:

- Inaamua uwakilishi katika Bunge la Marekani na kuathiri wilaya za kutunga sheria za ndani;
- Ni msingi wa kufadhili mipango na huduma muhimu; na
- Husaidia ufanyaji maamuzi ya karibu kwa ajili ya ustawi wa uchumi, miradi ya ujenzi wa shule na usafiri na pia mipango ya afya ya umma, usalama wa umma na dharura.

Kila mkazi wa Maryland ni Muhimu!

Hesabiwa katika Sensa ya Kila Baada ya Miaka Kumi ya 2020

Sensa ni Muhimu

Data ya sensa hutumiwa kuamua kiwango cha ufadhili wa serikali kuu kwa mipango kama vile Supplemental Nutrition Assistance Program for Women, Infants and Children (SNAP/WIC), Medicaid, Children's Health Insurance Program (CHIP) na miradi ya barabara kuu na usafiri.

- Kila mwaka, serikali kuu hutenga zaidi ya **Dola Bilioni 675** za ufadhili kulingana na data ya sensa.
- Kila mkazi wa Maryland ambaye hakuhesabiwa hugarimu jimbo takribani **Dola 18,250** kwa miaka 10 – hii ni sawa na jimbo kupoteza **Dola Bilioni 1** (kulingana na hesabu ya chini ya Sensa ya Marekani kihistoria).

Kujaza fomu yako ya sensa huhakikisha kuwa familia, jirani na jamii za Maryland zinapokea ufadhili zinaohitaji ili kuishi, kufanya kazi, kucheza na kukua.





Sensa ni Rahisi

Kujaza fomu yako ya sensa kunaweza kufanywa kwa njia tatu – **[kwa barua, simu au](#)**

[mtandaoni](#). Sensa ya 2020 itakuwa **sensa ya kwanza mtandaoni** katika historia ya Marekani.

Kujibu maswali ya demografia katika sensa husaidia kuhakikisha kuwa jamii yako inapokea **mgao sawa wa ufadhili** na kuwa maamuzi ya ustawi wa uchumi na mipango inaakisi kwa usahihi jamii yako tarehe 1 Aprili, 2020.

Baadhi ya mambo muhimu ya kufahamu. Usisahau:

- Wanafunzi wa chuoni wanapaswa kuhesabiwa kwenye anwani yao ya chuoni, kwenye bewa au nje ya bewa. Wanapaswa kuhesabiwa nyumbani kwa wazazi wao ikiwa tu wanaishi na kulala huko.
- Lazima watoto wote wahesabiwe **[ikiwemo wale walio chini ya miaka mitano](#)**.

Sensa ni Salama

U.S. Census Bureau **[lazima iweke taarifa zote siri](#)**, ikiwemo uraia wa mkazi, data ya mapato na nyingine ya binafsi ambayo ni nyeti.

- Data inakusanywa kwa madhumuni ya takwimu pekee na **[data ya binafsi haifichuliwi kamwe](#)**.
- Taarifa zote za sensa ni za siri na zinalindwa na sheria katika Title 13 ya Kanuni ya Marekani huku ukiukaji ukiadhibiwa kwa hadi miaka mitano katika gereza la serikali kuu na/au faini ya dola 250,000.

Kwa hivyo chagua njia ambayo utahesabiwa – kwa barua, simu au mtandaoni.

[Ni picha yetu ambayo itadumu miaka kumi, hivyo tumwezeshe kila mtu kuwa ndani.](#)



[Census.Maryland.gov](https://www.census.gov/maryland)

Barua pepe: Census@Maryland.gov • **Twitter:** [@MDCensus2020](https://twitter.com/MDCensus2020) • **Simu:** 410.767.4500



Larry Hogan, Gavana Boyd
Rutherford, Lt. Gavana
Robert S. McCord, Katibu Sandy
Schrader, Naibu Katibu

